

RASILIMALI KWA WAKIMBIZI

KUJIFUNZA KINGEREZA

kiwa hauseme kingereza kukuya na kuikala Amerika inaweza kukuogopesha saana. Kujitembeza inje, kupata kazi, hata kuenda uza mboga utabiona bigumu ikiwa kingereza yako ni ya kidogo saana. Alakini, kujifunza kingereza, mwisho itakusaidiya kuzoweya muzuri mgini kwenye unaishi. Hata ukuwe na myaka ngapi, ao ukuwe mwanaume ao mwanamuke, kujifunza kusema ao kusikiya kingereza itakusaidiya kuji simama ako, kupata kazi yenyi kulipa muzuri, kuweza kushirikiyana na ba rafiki piya ba jirani yako. Ikifika unapata kazi mbele ujuwe kingereza muzuri, utaendeleya kusoma na uko natumika. Wakati yote yenyi utakuwa haujuwe kingereza muzuri, utapewa interprete ukienda fasi sawa ku hopital, ao tribunal.

FAIDA ZA KUJIFUNZA KINGEREZA

Kingereza njo luga karibu batu bote banasema hapa Amerika na karibu batu bote hapa Amerika habataweza kusumuliya na weye ao kukusiya kama haujifunze kingereza. Kujifunza kingereza ni lazima kwako kwa kuweza ishi na kusonga mbele. Kama uko na batoto, kujuwa kingereza itakusaidiya kusumuliya na batumishi ya masomo ya batoto yako. Piya uko na lazima ya kujifunza kingereza njo usipitiwe na habari na ukuwe mkaaji mwenyi kujuwa habari za mgini na habari za inchi ndogo (Etat) kwenyi unaishi. Uko na lazima yakujifunza kingereza njo uweza mashindano yenyi utafanyaka wakati utaomba urahiya (Citoyenneté).



KUJIFUNZA KINGEREZA



Utajufunza kingereza mbiyo zaidi kama uko na niya saana ya kujuwa luga. Angaliya ju ya nini kujifunza kingereza iko ya lazima:

- Kupataka kazi na kuendeleya muzuri mu kazi.
- Kusumuliya na balimu ya batoto yako.
- Kujuwa batoto yako na banjukuu yako biko banasema nini.
- Kujisimama ako: kujuwa kukamata bisi, tram, train na kuenda kujihemeleya na kuhemeleya jamaa yako.
- Kusumuliya na ba jirani yako.
- Kujuwa nini iko napitikana mu dunia ukisikiliza télévision, ukisoma gazeti (Journal) na internet.
- Kuweza mashindano ya Amerika wakati unaomba urahiya (citoyenneté) wa Amerika.
- Kusumuliya na banzenu bakazi na batu bengine ndani mgini kwenyi unaishi.
- Kulomba kukutanana na docteur na kuenda kukutanana naye bila interprète.

MASOMO ZA KINGEREZA

Kuna shirka mingi zenyi kufundisha kingereza ku bageni na bakimbizi benyi banamaliza fika Amerika. Masomo zimoja zinapewa bure, Shirika yako ya kuhamishwa (Agence de réinstallation) itakusaidiya kukutafutiya fasi unaweza Someya pembedi ya kwenyi unaishi.

Ndani ya masomo za kingereza, banaume na banamuke ba kimwa mbalimbali na bakutoeya mu inchi mbalimbali bana ikalaka pamoya. Mu somo za mwanzo, banafundishaka banafunzi bitu bya tegetege, kingereza yakukusaidiya kidogo wakati unatembeaya inje. Kwa mfano, banaweza kufundisha misemwa (phrases) za kingereza za kukusaidiya tu kuuza bitu mu soko, kusoma programme ya bisi, ao kutafuta kazi. Masomo zingine zinafundisha

tu kingereza ya kukusaidiya kupata kazi fulani, sawa kutumika mu hôtel ao kutumika fasi banatunza bagonjwa. Mu somo za yulu, banafunzi bajifunza zaidi grammaire ya kingereza, kusoma, na kuandika. Kuna

piya masomo za kingereza zenyi kutayarisha banafunzi kuenda ku college.

NAMNA ZINGINE ZA KUJIFUNZA KINGEREZA

Kuko namuna mingi za kujifunza kingereza. Mara mingi ni muzuri kuchanga namuna za kujifunza kingereza. Sikiliza namna gani unaweza jifunza kingireza wakati hauende kumasomo:

Cultural Orientation Resource Exchange

8719 Colesville Road, 3rd Floor • Silver Spring, MD 20910

For more information, visit the CORE Resettlement Navigator website at corenav.org.



The contents of this fact sheet were developed under an agreement financed by the Bureau of Population, Refugees, and Migration, United States Department of State, but do not necessarily represent the policy of that agency and should not assume endorsement by the Federal Government. **This material is in the public domain and may be reproduced.**

Unaweza jifunza kingereza ku kazi: Wakati unapata kazi unaweza jifunza maneno na misemwa za kingereza zenyi zitakusaidiya mu kazi. Utakuwa na benzenu ba kazi na inawezekana piya batu benyi kuya kuuza ao kuuzisha benyi kujuwa kingereza. Kusumuliya nabo itakusaidiya kukaza kingereza yako.

Ujifunze Kingereza mu muji kwenyi unaishi. Ufungule roho yako na ufurahiye kukutanana na batu ba mupya. Kusumuliya na batu benyi haujuwe mu maduka na kusumuliya kingereza na ba rafiki ao ba jirani unaweza iona nguvu ku mwanzo, alakini batu mungu batakukaribisha na batajikaza kukusaidiya. Ujiandikishe ao wepeke uanzu kundi mu quartier yakujifunza kingereza ao ya kujulishana tabiya za inchi kwenyi munatoka na mukutanane mara mungu kila wakati kwakusema tu mu kingereza. Upange bitu byenyi munapendaka kama kundi, sawa kuenda ku musée ao kuenda tembeya mu parc. Hiyo itakuwa namna muzuri ya kujifunza kingereza pamoja na batu bengine benyi kujifunza ao benyi kukiwa muzuri. Na hiyo inaweza kuwa namna muzuri ya kujifunza tabiya na mila (Culture) za Amerika.

Kujifunza wepeke. Ujitiye moyo wepeke kwa kujifunza kingereza fasi yoyote ao wakati yoyote zenyi inawezekana. Unaweza jifunza wepeke ukiangaliya ma sinema ao michezo ku télévision ao mukusikiliza programmes za kingereza ku radio. Andika maneno zote za mupya zenyi ulijifunza na ujikaze kusoma zenyi kuandikiwa ku barabara, ku ma bisi, na kumadirisha ya ma duka (Magasins).

Kujifunza kama jamaa.

Kila mutu ndani ya jamaa atakuwa anajifunza kingereza pamoya na weye. Uifanye kuwa kitu ya kujifurahisha ndani ya jamaa mukifanya michezo za kingereza na kila siku mijipatiye ndani ya jamaa wakati Fulani ya kusema "kingereza tu". Utumike pamoya na masomo ya mtoto wako ukienda saidiya ndani ya hiyo somo ao kama kuna bya lazima saana bilifanyika ku masomo. Batoto banajifunzaka luga mbiyo saana, ni lazima basikuache nyuma saana.



KUJIFUNZA KINGEREZA INACHUKUWAKA MUDA (WAKATI)

Ku mwanzo, unaweza ona kama kujifunza kingereza iko nguvu na unaweza jisikiya unachanganyikiwa. Ni kawaida kujisikiya unachanganyikiwa. Kila mutu anajifunza mbiyo ao polepole na kila mutu anajifunza namuna mbalimbali. Upime namuna mbalimbali na utumikishe namna yenyi unaona inakusaidiya zaidi. Siri ya Kujuwa luga ya mupya ni kujifunza kusema na kuandika kila siku. Hata ikiwa unasihiyaka radio, ao unaangaliyaka télévision mu kingereza hata 10 minites kila siku itakusaidiya. Wakati ikisha pita na pamoja na hiyo kusema utajisikiya huru zaidi kusema kingereza na hiyo itakusaidiya kuzoweya bila magumu mingi maisha ya America. Itakamata wakati alakini bitakuwa byepesi kama unaendeleya kujikaza.